# Usafiri ARDHINI

ISSN 2961 - 6255 OKTOBA - DESEMBA, 2025 Toleo la 9




## MHE. KIHENZILE: NCHI YETU NI SALAMA, KARIBUNI MUWEKEZE

“Tunahitaji wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili wawe sehemu ya ustawishaji wa sekta ya usafiri ardhini nchini na kwa kufanya hivyo watakuwa wameunga mkono jitihada za Serikali za kuboresha na kurahisisha....”

Uk 5

## WATANO MBARONI KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI

“Timu ya ukaguzi imebaini watu wenye tiketi mkononi zisizo halali kuanzia 20 hadi 30 zenye nauli kubwa na abiria wamekuwa wakiuziwa tiketi za safari za mabasi kwa bei ya juu na wakifika kwenye mabasi wanakuta nauli halisi ni ndogo.....’

Uk 13

# DKT. NCHEMBA: SEKTA YA USAFIRISHAJI NI UTI WA MGONGO WA UCHUMI

Uk 8

# TAHARIRI



CPA DKT. HABIBU SULUO
MKURUGENZI MKUU - LATRA

Sekta ya usafiri ardhini inaendelea kuwa nguzo muhimu katika kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii. Serikali, kupitia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali, imeendelea kuwekeza kwa makusudi katika miundombinu na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuhakikisha huduma za usafiri ardhini zinakuwa bora, salama na endelevu.

Toleo la tisa la jarida la USAFIRI ARDHINI linaangazia mafanikio yaliyopatikana kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025. Taarifa zilizomo zimekusanywa na kuhaririwa kwa lengo la kuonesha jinsi maboresho ya kiutendaji, matumizi ya teknolojia na ubunifu yanavyoendelea kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma. Kupitia kurasa zilizopo ndani ya Jarida, utafahamu mafanikio yaliyopatikana katika sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ikiwa ni matokeo ya usimamizi madhubuti na uwajibikaji unaozingatia matokeo.

Mwezi Novemba 2025, uliweka alama ya kipekee katika historia ya LATRA kwa kuadhimishwa kwa mara ya kwanza Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini. Maadhimisho hayo yalifunguliwa rasmi na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 26, 2025 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC). Huku, Mhe. David Kihenzile (Mb) Naibu Waziri wa Uchukuzi, akifungua maonesho yaliyofanyika kuanzia Novemba 24 hadi 29, 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali wa usafirishaji walitunukiwa tuzo za utoaji huduma bora na salama, ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wao katika kuboresha sekta ya uchukuzi nchini.

Sambamba na hilo, LATRA imeendelea kuimarisha udhibiti wa huduma kwa kufanya kaguzi za kushtukiza katika vituo vya mabasi nchini, hususan kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka 2025. Hatua hii imelenga kuhakikisha watoa huduma wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Usafiri Ardhini, na hivyo kuwalinda abiria dhidi ya bughudha na kuhatarisha usalama wao.

Vilevile Mamlaka imeendelea kujipambanua kwa utendaji bora ambapo Desemba 17, 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Mhe. Joseph Mkude, Mkuu wa Wilaya ya Arusha aliyemuwakilisha mgeni rasmi Mhe. Makame Mbarawa (Mb) Waziri wa Uchukuzi, aliitangaza LATRA mshindi wa kwanza miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25. Mafanikio haya yanathibitisha dhamira ya Mamlaka katika kutoa huduma kwa viwango vya juu vya ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

Karibu usome jarida hili kupata taarifa, elimu na uelewa wa kina kuhusu mageuzi yanayoendelea katika sekta ya usafiri ardhini. Kwa maoni, ushauri au malalamiko, wasiliana nasi bila malipo kupitia namba 0800 110019 au 0800 110020, tumia Mfumo wa e-Mrejesho, au tembelea ofisi ya LATRA iliyo karibu nawe. Unaweza pia kutuma picha au video zinazoonesha uvunjifu wa Sheria za Usafiri Ardhini kupitia namba ya WhatsApp 0681 300800 nasi tutazifanyia kazi kwa wakati.

Nikutakie usomaji mwema wa jarida hili

*"Pamoja kwa Usafiri Bora"*

# TANZANIA KUADHIMISHA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI




Kwa mara ya kwanza, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inaadhimisha Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini itakayofanyika Dar es Salaam Novemba 24 hadi 29, 2025 kwa kaulimbiu ya 'Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji'.

Hayo yamebainishwa na Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi hivi karibuni ambapo amesema maadhimisho hayo yataambatana na maonesho yatakayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja pamoja na makongamano yatakayofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) na kuhusisha wadau wa usafirishaji kutoka ndani na nje ya nchi.

"Nawakaribisha wadau wa sekta ya Uchukuzi katika tukio la kwanza la aina yake na kwa upande wa Tanzania maadhimisho haya ni muhimu kwani yanatoa fursa kwa wadau kushuhudia mageuzi makubwa yaliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta ya uchukuzi, hususan kwenye uwekezaji wa miundombinu ya kisasa kama reli, bandari na barabara," amesema Prof. Kahyarara.

Vilevile amesema kuwa, ajenda ya Nishati Safi ni kipaumbele kikubwa cha Serikali ambapo Tanzania imepiga hatua kubwa kupitia miradi ya Reli ya Kisasa (SGR) inayotumia umeme, na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika bandari.

"Tanzania ina Reli ndefu zaidi kuliko nchi zote Afrika ambayo inatumia Nishati safi ya umeme kupitia mradi wa SGR unaogharimu zaidi ya shilingi trilioni 40 na utakapokamilika utakuwa na urefu wa kilomita 10,707, ukianzia



*Inaendelea Uk 2 >>*

# TANZANIA KUADHIMISHA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI

*<< Inatoka Uk 1*

Dar es Salaam hadi Mwanza, Kigoma, Burundi, DRC, Kigali na Uganda. Sekta ya usafirishaji inachangia takribani asilimia 40 ya mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na asilimia 98 ya biashara za ndani na nje, hivyo ni injini muhimu ya uchumi wetu," ameeleza Prof. Kahyarara.

Naye CPA, Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA ameeleza kuwa, uaandaaji wa maonesho yanahusisha utekelezaji wa azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) na kwa kutambua juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kufanikisha Mkakati wa Taifa wa matumizi ya Nishati safi.

"Mkumbuke kwamba, Rais aliibeba ajenda ya nishati safi na kwa kutimiza hilo kaulimbiu ya mwaka huu inasisitiza jukumu muhimu la mifumo ya usafiri shirikishi, yenye ustahimilivu na rafiki kwa mazingira katika kufanikisha maendeleo endelevu ya nchi, na katika wiki hiyo kutakuwa na maonesho ya sekta ya usafiri, mijadala, semina na mafunzo mbalimbali yatakayohusisha wadau kutoka ndani na nje ya nchi," ameeleza CPA Suluo.

Kwa upande wake Bw. Plasduce Mbossa, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) amesema kuwa, sekta ya bandari inategemea sana ushirikiano na miundombinu ya barabara na reli ili kuongeza ufanisi wa shughuli za usafirishaji nchini.

"Shughuli zetu za bandari zinahitaji kuwa na viunganiko na sehemu ambazo tutawafikia wateja kwa kutumia usafiri wa reli na barabara, mategemeo ni kwamba ujenzi unaoendelea wa reli ukikamilika utaongezea ufanisi zaidi wa bandari zetu kusafirisha mizigo kwa wingi, kwa sasa tunahudumia zaidi ya tani milioni 32 kwa mwaka, mafanikio haya ni matokeo ya uwepo wa njia bora za kuunganisha bandari na masoko ya ndani na nje," amesema Bw. Mbossa.

Mhandisi Machibya Masanja, ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambaye ameeleza kuwa, TRC imejizatiti kuhakikisha miundombinu ya reli inarahisisha utoaji wa huduma bora za usafirishaji wa mizigo na abiria.

"Tunashukuru Serikali kwa uwekezaji mkubwa katika mradi wa treni za kisasa (SGR) unaoendelea kwa urefu wa kilomita 2,102 katika awamu ya kwanza. Mradi huu utapunguza gharama za usafirishaji na kuongeza ufanisi. Kaulimbiu ya 'Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji' inajidhihirisha kwa vitendo kupitia huduma zetu zinazotumia Nishati mbadala ya umeme badala ya mafuta," amesema Mha. Masanja.

Kimataifa siku ya Usafiri Endelevu Duniani huadhimishwa tarehe 26 Novemba kila mwaka kwa lengo la kutathmini maendeleo ya sekta ya usafiri duniani na kuhimiza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira. Maadhimisho haya yanatoa fursa kwa wadau mbalimbali wa usafirishaji hapa nchini kushiriki kwa kuwa na mijadala, kubadilishana uzoefu na kujifunza namna bora ya kutoa huduma bora.

> **"Tanzania ina Reli ndefu zaidi kuliko nchi zote Afrika ambayo inatumia Nishati safi ya umeme kupitia mradi wa SGR unaogharimu zaidi ya shilingi trilioni 40 na utakapokamilika utakuwa na urefu wa kilomita 10,707**
>
> *Prof. Godius Kahyarara,*

# DKT. NCHEMBA ATUNUKU TUZO ZA WATOA HUDUMA BORA NA SALAMA ZA USAFIRI ARDHINI




*Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwatunuku wadau wa usafirishaji tuzo ya utoaji huduma bora na salama kwenye ufunguzi wa Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2025 yaliyofanyika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam Novemba 26, 2025*

Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewatunuku wadau wa usafirishaji tuzo ya utoaji huduma bora na salama zilizoshindanishwa kuanzia Juni 2024 hadi Julai 2025 kwa lengo la kutambua na kuthamini michango ya wadau hao katika sekta ya Uchukuzi.

Dkt. Nchemba amekabidhi tuzo hizo kwenye ufunguzi wa Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2025 iliyoandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na kufanyika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam Novemba 26, 2025 ambapo alikuwa mgeni rasmi wa Maadhimisho hayo.

Akizungumza mbele ya Mhe. Dkt. Nchemba, CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kimeipa LATRA wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa. Ameeleza kuwa, utoaji wa tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama, ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu huo ambapo wameshindanisha watoa huduma kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Juni 2025.

"Vigezo vilivyotumika kuwapata washindi kwa mujibu wa Sheria na kanuni ni pamoja na usimamizi wa vyombo vya usafiri pamoja na wafanyakazi, Ubunifu na matumizi ya teknolojia, Usalama na huduma bora kwa wateja, Matumizi ya madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA,

*Inaendelea Uk 4 >>*

# DKT. NCHEMBA ATUNUKU TUZO ZA WATOA HUDUMA BORA NA SALAMA ZA USAFIRI ARDHINI

*<< Inatoka Uk 3*

Utunzaji wa mazingira, ulipaji wa tozo za LATRA kwa wakati sahihi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Usafirishaji, Bima na Usalama Barabarani," amesema CPA Dkt. Suluo.

Pia CPA Dkt. Suluo amesema upatikanaji wa washindi hao umehusisha zoezi la mchunjo kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza washindani walichujwa kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa na awamu ya pili ilihusisha kura zilizopigwa na watumia huduma za usafiri ardhini.

Jumla ya makundi saba yametunukiwa tuzo hizo ambao ni wasafirishaji kwa magari ya mizigo ndani ya nchi na nje ya nchi, Wasafirishaji kwa mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani), Madereva wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani), Wahudumu wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani), Watoa huduma za mifumo ya Tiketi Mtandao (e-Tickets Vendors), Watoa huduma ya Mifumo ya Ufuatiliaji Mwenendo wa Magari (VTS) na Watoa huduma ya mifumo ya Teksi mtandao (Ride Hailing Platforms) inayojumuisha jumla ya washindi 27.



*Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifungua rasmi Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini Novemba 26, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam*

*Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akipatiwa maelezo na mmoja wa waoneshaji wa Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025, kuhusu namana bidhaa zao zinavyofanya kazi katika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam Novemba 26, 2025*



# MHE. KIHENZILE: NCHI YETU NI SALAMA, KARIBUNI MUWEKEZE




*Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi akikata utepe kuashiria ufunguzi wa maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, Novemba 24, 2025. Kulia ni Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA.*

Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) Naibu Waziri Uchukuzi amewakaribisha wadau wa sekta ya usafiri ardhini kuwekeza kwenye sekta ya usafirishaji kwa kuwa nchi ni salama na mazingira ya uwekezaji yameboreshwa.

Mhe. Kihenzile amesema hayo Novemba 24, 2025 alipofungua maonesho ya Maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yanayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam.

“Nchi yetu ni salama na tunahitaji wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili wawe sehemu ya ustawishaji wa sekta ya usafiri ardhini nchini na kwa kufanya hivyo watakuwa wameunga mkono jitihada za Serikali za kuboresha na kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji nchini,” amesema Mhe. Kihenzile.

Vilevile amewasihi watanzania kuipenda na kuithamini nchi yao huku wakitunza miundombinu ya usafirishaji iliyojengwa na iliyoboreshwa na Serikali kupitia uwekezaji mkubwa uliofanyika kwa nia njema ya kushughulikia changamoto za usafiri nchini.

“Serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji hivyo ni jukumu la kila mwananchi kuilinda na kuitunza kwa kuwa inasaidia katika kukuza uchumi. Kuharibu miundombinu iliyopo kunaleta athari sio kwa Serikali pekee bali kwa wananchi na wasafirishaji ambao wamewekeza katika huduma za usafiri na usafirishaji na hivyo kurudisha nyuma maendeleo,” ameeleza Mhe. Kihenzile.

Maonesho ya Maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yanafanyika Novemba 24 hadi 29, 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam ambapo wadau wa usafirishaji kutoka ndani na nje ya nchi wanatoa elimu ya majukumu yao pamoja na huduma kwa wananchi.

# JUMUIYA YA SARA YAKOSHWA NA UBORESHAJI WA USAFIRI WA RELI TANZANIA



Bw. Raymond Shoniwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Reli Kusini mwa Afrika (SARA) amesema wamekoshwa na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuboresha sekta ya usafiri wa reli jambo ambalo limerahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Bw. Shoniwa amebainisha hayo Novemba 24, 2025 wakati wa ufunguzi wa maonesho ya Maadhmisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yanayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam ambapo wadau wa usafirishaji wa ndani na nje ya nchi wanatoa elimu na huduma kwa wananchi wanaotembelea viwanjani hapo.

“Nawapongeza sana kwa hatua hii mliyofikia na tunatambua kazi nzuri mnayoifanya kwenye uwekezaji hasa wa sekta ya usafirishaji hasa kwenye usafiri wa reli na kwa haya mnayoyafanya mwakani tutafanya vikao vyetu vya Bodi hapa Tanzania ili na sisi tujifunze zaidi,” ameeleza Bw. Shoniwa.

Kwa upande wake. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) Naibu Waziri wa Uchukuzi amesema moja ya maeneo ambayo Serikali imeboresha kwenye upande wa usafiri wa reli ni mabadiliko ya Sheria ya Reli ambayo kwa sasa inaruhusu wawekezaji wa sekta binafsi ndani na nje ya nchi kutoa huduma za usafiri wa reli kwa kutumia miundombinu ya Serikali iliyopo.

“Serikali imeruhusu jambo hili ili kutoa fursa kwa kampuni binafsi kuwekeza kwenye usafirishaji kwa sababu miundombinu inayowezesha huduma hii ipo na tunaamini jambo hili litainua uchumi wa wananchi na Taifa kwa jumla,” amesema Mhe. Kihenzile.

Tanzania inaadhimisha kwa mara ya kwanza Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini kuanzia Novemba 24 hadi 29 Dar es Salaam ambapo inahusisha maonesho katika viwanja vya Mnazi Mmoja na makongamano yatakayofanyika Novemba 25 hadi 27, 2025 ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo kwa mwaka 2025 ni Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji.

# BODI YA LATRA YAPONGEZWA KWA KUANDAA MAADHIMISHO YA KWANZA YA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI



*Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi akizungumza katika ufunguzi wa maonesho ya Maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, Novemba 24, 2025.*

Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) Naibu Waziri wa Uchukuzi ameipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kutekeleza maelekezo ya kuandaa maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yanayofanyika Novemba 24 hadi 29, 2025 Dar es Salaam.

Mhe. Kihenzile ametoa pongezi hizo Novemba 24, 2025 alipofungua maonesho ya Maadhmisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yanayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam na kuhusisha wadau wa usafirishaji wa ndani na nje ya nchi wanaotoa elimu na huduma kwa wananchi wanaotembelea viwanjani hapo.

"Tunawapongeza kwa kutekeleza agizo hili kwa ubunifu mkubwa na kupitia wiki hii, tutajifunza jinsi matumizi ya nishati safi yanavyotunza mazingira na kupunguza gharama za usafirishaji na pia tutaona ubunifu wa mifumo ya sekta ya usafirishaji inavyorahisisisha utoaji wa huduma kwa wananchi," amesema Mhe. Kihenzile.

Vilevile ameipongeza LATRA kwa kazi nzuri ya udhibiti usafiri ardhini inayoifanya ambapo kwa sasa ushirikiano na wadau umeongezeka na mifumo ya kiudhibiti inafanya kazi ambayo inarahisisha utoaji wa huduma kwa wadau ambao ndio watumiaji wa huduma hizo.

Naye Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA ameishukuru Wizara ya Uchukuzi kwa usimamizi wa karibu kwa LATRA uliochangia kufanikisha kwa ufanisi utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa.

Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini inaadhimishwa Novemba 24 hadi 29 Dar es Salaam na maadhimisho hayo yanafanyika sambamba na Siku ya Usafiri Endelevu Duniani inayoadhimishwa Novemba 26 kila mwaka. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo kwa mwaka 2025 ni Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji.

# DKT. NCHEMBA: SEKTA YA USAFIRISHAJI NI UTI WA MGONGO WA UCHUMI

Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema kuwa sekta ya usafirishaji ni sekta wezeshi katika kukuza uchumi wa Tanzania na duniani kwa jumla.

Dkt. Nchemba mesema hayo alipofungua rasmi Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini Novemba 26, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam (JNICC) ambapo alikuwa mgeni rasmi wa Maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

“Sekta ya usafirishaji ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yetu, tuitunze miundombinu ya usafiri na sote ni mashahidi kuwa miundombinu hii ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu. Hatuwezi tukapiga hatua ya maendeleo bila kuitunza, ni mali yetu sote ni chanzo kikubwa cha maendeleo ya mtu mmoja mmoja,” amesema Dkt. Nchemba.

Naye Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi amesema kuwa, shughuli zote zinazotekelezwa zinategemea sekta ya usafirishaji ambapo wananchi husafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine ili waweze kutimiza mahitaji yao muhimu na uendeshaji wa shughuli zote za kiuchumi.

Vilevile amesema, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya usafirishaji, Wizara kwa kushirikiana na LATRA inahakikisha masuala ya nishati safi yanapewa kipaumbele katika shughuli za usafiri na usafirishaji nchini kupitia barabara na reli.

“Wizara itaendelea kuwakaribisha wadau wakiwemo mashirika ya maendeleo na

*Inaendelea Uk 9 >>*



*Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitoa hotuba, alipofungua rasmi Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini Novemba 26, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam*

## DKT. NCHEMBA: SEKTA YA USAFIRISHAJI NI UTI WA MGONGO WA UCHUMI

*<< Inatoka Uk 8*

taasisi binafsi na sekta bunifu kushirikiana na Serikali kuhakikisha masuala ya nishati safi yanapewa kipaumbele katika sekta ya usafiri na usafirishaji ili kukuza uchumi," amesema Prof. Mbarawa.

Ameongeza kuwa, kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi ya nishati safi katika usafiri ardhini nchini, Tanzania inaendesha usafiri wa reli ya kisasa (SGR) kwa kutumia nishati safi ya umeme na matumizi ya nishati ya gesi kwa usafiri wa mabasi yaendayo haraka (BRT).

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji na yamejumuisha maonesho yaliyofanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja na Makongamano yaliyofanyika JNICC Novemba 24 hadi 29, 2025 ambapo wadau mbalimbali walikutana kujadili na kujifunza masuala yanayohusu sekta ya usafirishaji katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

## WADAU WA USAFIRISHAJI WAASWA KUTII SHERIA

Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewasihi wadau wa sekta ya usafiri ardhini nchini wakiwemo watoa huduma na watumiaji wa huduma za usafiri kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini zilizopo ili kupunguza ajali zinazoweza kuepukika.

Dkt. Nchemba amebainisha hayo alipofungua rasmi Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025, Novemba 26, 2025 Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam.

"Nitoe rai kwa wadau wote kutekeleza Sheria za usafirishaji nchini pamoja na kuitunza miundombinu iliyotengenezwa na kuboreshwa na Serikali kwa gharama kubwa. Miundombinu hii inawawezesha wananchi kuinua uchumi wao kupitia biashara ya usafirishaji abiria na mizigo," ameeleza Mhe. Nchemba.

Wakati huohuo, Dkt. Nchemba amezitaka taasisi zinazohusika na kusimamia Sheria za usafirishaji zilizowekwa kwa ajili ya wananchi kuhakikisha Sheria hizo zinasimamiwa vizuri na kutekelezwa bila kubagua.

Kwa upande wake CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa LATRA itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo, na itaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani katika kutekeleza majukumu yake, hususan kupambana na ajali za barabarani.

Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini imeipa LATRA jukumu la kudhibiti sekta ndogo tatu ambazo ni sekta ya usafiri wa barabara, usafiri wa reli na usafiri wa waya.



*Viongozi na wadau mbalimbali wa Usafiri nchini wakiongozwa na Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakiimba wimbo wa Taifa wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya kwanza ya WIki ya Usafiri Endelevu Ardhini Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Novemba 26, 2025*

>>




*CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), akikagua taarifa zilizopo kwenye tiketi ya kielektroni wakati wa ukaguzi wa mwisho wa mwaka, Desemba 6, 2025 Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli, Dar es Salaam.*

<<



*CPA Njama Moyo, Afisa Mhasibu Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), akipokea tuzo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu LATRA baada ya LATRA kuibuka mshindi wa tatu (kundi la Mamlaka za Udhibiti) katika Tuzo za Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), kwa uwasilishaji Bora wa Hesabu za Kifedha katika Sekta ya Umma kwa viwango vya Kimataifa (IPSAS) mwaka 2024, , Desemba 04, 2025 Ukumbi wa Mikutano APC Bunju, Dar es Salaam.*

>>

# CPA SULUO: WATEJA NI KIPAUMBELE CHETU



*CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu (LATRA) akimhudumia mteja aliyetembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja Oktoba 8, 2025*

CPA, Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema LATRA inathamini na inatambua mchango wa wateja katika kuboresha huduma na utendaji kazi wa Mamlaka na wao ndio kipaumbele cha Mamlaka hiyo.

CPA Suluo ameeleza hayo ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Oktoba 08, 2025 kwenye maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja yanayofanyika Oktoba 06 hadi 10, 2025 ambapo aliwahudumia wateja kikamilifu, kusikiliza maoni na kutatua changamoto za wateja waliotembelea ofisi hiyo.

"Wateja ni namba moja kwetu na sisi tupo kwa ajili ya kuwahudumia, endapo hawajaridhika na huduma za Mamlaka wawasilishe maoni au malalamiko yao kwa namba bila malipo 0800110019 au 0800110020 au kupitia mfumo wa eMrejesho, pia wawasilishe video za ushahidi wa vitendo vyote vinavyofanyika kwenye usafiri wa umma ambavyo vinavunja Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini nasi tutapokea na kufanyia kazi", amesema CPA Suluo.

Vilevile amebainisha kuwa, Mamlaka imebuni na kutengeneza mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kurahisisha utendaji kazi wa Mamlaka na utoaji wa huduma za usafiri ardhini nchini.

"Wateja wetu wanaweza kuomba, kupata na kuhuisha leseni za usafirishaji kwa mtandao kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Reli na Barabara (RRIMS) rrims.latra.go.tz/, wanaweza kukata tiketi za Treni na Mabasi kwa mfumo wa Safari Tiketi tiketi.latra.go.tz/ kufahamu nauli halali za magari ya mijini (daladala) na mabasi yanayoenda mkoani kwa kupakua LATRA APP inayopatikana Play Store. Pia kwa sasa vituo vya mabasi vipo kiganjani kupitia Mfumo wa


*Inaendelea Uk 12 >>*

## CPA SULUO: WATEJA NI KIPAUMBELE CHETU

*<< Inatoka Uk 11*

Taarifa kwa Abiria pis.latra.go.tz/," ameeleza CPA Suluo.

Kaulimbiu ya Wiki ya Huduma kwa Wateja ni "Mission Possible" yaani "Mipango Imewezekana" ambapo mipango ya LATRA ya kuboresha uduma zake imewezekana kupitia mifumo ya TEHAMA pia imeweza kusogeza huduma zake karibu na wadau kupitia ofisi zake zinazopatikana kote Tanzania Bara.

0800110019
0800110019

VTS

tiketi.latra.go.tz

DTS

emrejesho.gov.go.tz

PIS

rrims.latra.go.tz

## HUDUMA ZA USAFIRI WA UMMA KUENDLEA KUTOLEWA SIKU YA UCHAGUZI MKUU

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeeleza kuwa, huduma za usafiri wa umma siku ya Uchaguzi Mkuu Oktoba 29, 2025 zitaendelea kutolewa kama kawaida.

Hayo yamebainishwa na Bw. Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA alipozungumza na wanahabari, ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Oktoba 24, 2025 kuhusu utoaji wa huduma za usafiri wa abiria siku ya Uchaguzi Mkuu.

Bw. Silanda amesema kuwa, wapo baadhi ya wapiga kura watakaohitaji kutumia usafiri wa umma ili kufika kwenye vituo vya kupigia kura, hivyo ni wajibu wa Mamlaka kuwezesha jambo hilo pasi na changamoto yoyote.

"Hadi sasa hakuna msafirishaji yeyote aliyewasilisha maombi rasmi ya kusitisha huduma siku ya uchaguzi hivyo tunawasihi wasafirishaji kuendelea kutoa huduma na wananchi waendele kutumia huduma za usafiri wa umma na watumie haki yao ya msingi kikatiba ya kupiga kura," amesema Bw. Silanda

Kwa upande wake, Bw. Issa Nkya, muweka hazina wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) amesema wamejipanga kutoa huduma za usafiri na usafirishaji na wananchi waondoe shaka kuhusu usafiri kwa kuwa unapatikana saa 24.

"Sisi kama wasafirishaji tumezungumza na tumekubaliana kuendelea kutoa huduma siku ya uchaguzi ingawa baadhi ya makampuni watapunguza idadi ya magari kutokana na idadi ya abiria watakaokuwepo," ameeleza Bw. Lema

Mamlaka ina wajibu wa kufuatilia huduma za usafiri ardhini na kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa ukamilifu kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Usafiri Ardhini nchini.

# WATANO MBARONI KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI




Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewatia mbaroni mawakala watano wasio rasmi kwa kosa la kukiuka masharti ya leseni ikiwemo kutoza nauli kuliko kiwango kilichopangwa na Mamlaka pamoja na kutotoa tiketi za kielektroni.

Akizungumza na waandishi wa habari Desemba 6, 2025 Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli Dar es Salaam baada ya ukaguzi wa kushtukiza, CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, Mamlaka imefikia hatua hiyo baada ya kuwabaini mawakala ambao hawajasajiliwa na LATRA maarufu kama masarange wanaowadanganya abiria wa mabasi ya masafa marefu kwa kuwauzia tiketi za makaratasi zisizo halali.

"Timu ya ukaguzi imebaini watu wenye tiketi mkononi zisizo halali kuanzia 20 hadi 30 zenye nauli kubwa na abiria wamekuwa wakiuziwa tiketi za safari za mabasi kwa bei ya juu na wakifika kwenye mabasi wanakuta nauli halisi ni ndogo au basi walilokatiwa tiketi halipo kabisa, watuhumiwa hao tayari wapo chini ya ulinzi na taratibu za kuwafikisha katika vyombo vya Sheria unaendelea," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Vilevile amesema kuwa, baadhi ya kampuni za mabasi zilizohusika kuwatoza abiria nauli zaidi ya iliyoelekezwa na LATRA ni kampuni ya Haji's na Takbiir zinazofanya safari za Dar es Salaam - Lushoto ambapo Mamlaka imewaelekeza kurejesha nauli za abiria ambao wamewazidishia na huku wakitozwa faini kama sehemu ya adhabu ya makosa yao.

Kwa upande wake Bruno Samweli, abiria kutoka Mbagala Rangi Tatu akisafiri kuelekea Kahama amesema, kumekuwa na changamoto kutokana na uwepo wa walanguzi wa tiketi ambao hununua tiketi mtandaoni kisha kuuza kwa bei isiyoelekezwa na Mamlaka na amewashauri wanaokiuka taratibu hizo kufuata Kanuni na Sheria za leseni zao ili kuepusha kujiingiza kwenye

*Inaendelea Uk 14 >>*

## WATANO MBARONI KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI

*<< Inatoka Uk 13*

makosa yasiyo ya lazima .

Naye Sophia Kanengene, Msafiri kutoka Mbezi Luis kuelekea Geita – Katoro abiria aliyezidishiwa nauli ameishukuru Mamlaka kwa hatua waliyoichukua ya kuwakamata watuhumiwa hao na kuwapambania abiria waliozidishiwa nauli kurejeshewa nauli zao kwani wamekuwa wakitoza fedha nyingi bila wao kujua.

Kwa upande wao mawakala waliotiwa mbaroni wamekiri kutoza nauli isiyoidhinishwa na LATRA na kuwa wamewarejeshea abiria nauli zao baada ya kuwajibishwa na LATRA na wamewasihi mawakala wenzao kujitokeza kusajiliwa rasmi na LATRA na kuachana na vitendo hivyo.

Mamlaka inaendelea kufanya kaguzi mbalimbali mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za usafiri ardhini zilizokuwa bora na salama.

---

## CPA, DKT. SULUO: TUMIENI SAFARI TIKETI KUEPUKA ULANGUZI WA NAULI

CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewaasa abiria wa mabasi ya masafa marefu kutumia Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaojulikana kwa jina la Safari Tiketi https://tiketi.latra.go.tz/ kukata tiketi zenye nauli halali zilizoidhinishwa na Serikali kupitia LATRA ili kuepuka ulanguzi wa nauli unaosababisha migogoro baina ya abiria na wasafirishaji inayotokana na malipo ya pesa taslimu.

Dkt. Suluo amebainisha hayo alipofanya ukaguzi wa kushtukiza katika Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli Desemba 6, 2025 Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha hali ya huduma za usafiri zinaimarika kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Vilevile amewataka abiria kuthibitisha malipo ya tiketi zao kwa kutumia Mfumo Tumizi wa LATRA App unaopatikana kupitia Play Store na App Store kwenye Simu janja na kuwasiliana na LATRA bila malipo kwa namba 0800110019 au 0800110020 kwa changamoto yoyote wanayokutana nayo pindi wanapokata nauli za mabasi.

CPA, Dkt. Suluo amefafanua kuwa, katika ukaguzi huo Mamlaka imebaini kuwepo kwa watu wanaowalaghai abiria kwa kuwaandikia tiketi za makaratasi zisizo rasmi na kuwatoza nauli kinyume na Taratibu zilizopo.

“Katika ukaguzi uliofanyika Mamlaka imebaini baadhi ya watu wamekuwa wakifanya udanganyifu kuwa ni mawakala wa ukataji tiketi za mabasi na kuwatoza nauli kinyume na Sheria, watu hao wanakuwa na tiketi hadi 30 kutoka kampuni mbalimbali za mabasi na kuziuza kwa bei isiyo elekezi huku wakiwapeleka abiria kwenye mabasi ambayo hawayafahamu,” amesema CPA, Dkt. Suluo.

Pia CPA, Dkt. Suluo amewasisitiza abiria kuweka taarifa zao muhimu kwenye tiketi ikiwemo, Jina la abiria, namba ya basi, tarehe na muda wa safari, kituo cha kuanzia na kumalizia safari, nauli iliyolipwa, anwani na namba za simu za msafirishaji na namba ya tiketi husika.

Naye Bi. Upendo Nestory, abiria aliyezidishiwa nauli ameishukuru Mamlaka

*Inaendelea Uk 15 >>*

## CPA, DKT. SULUO: TUMIENI SAFARI TIKETI KUEPUKA ULANGUZI WA NAULI

*<< Inatoka Uk 14*

kwa kazi nzuri inayoifanya hasa ya kutetea abiria, "Nimefurahi sana mmekuja hapa kutusaidia, kiukweli sisi wananchi tulikuwa tunanyanyasika sana, na tulikuwa hatuna budi kulipa kiasi kilichozidi kwa sababu tulikuwa hatujui nini cha kufanya na tunaitaka safari, mimi namshukuru sana Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wote, kwa hili la leo nimeamini kuwa wanatuona na wanatusaidia," amesema Bi. Upendo.

Ukaguzi wa mwisho wa mwaka unaendelea mikoa yote Tanzania Bara ili kuhakikisha wasafirishaji na watoa huduma wanafuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Usafiri Ardhini huku abiria wakisafiri bila bughudha wakifurahia huduma za usafiri nchini.

---

## MAGOMBANA: KANUNI HIZI NI MUHIMU KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRISHAJI

Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa njia ya Barabara Wizara ya Uchukuzi amesema rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026 ni nyenzo muhimu ya kuimarisha sekta ya usafirishaji nchini,

Bw. Magombana amesema hayo Januari 8, 2026 katika mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026, ukumbi wa Mikutano Chuo cha Utalii Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Bw. Magombana ameeleza kuwa zipo changamoto mbalimbali katika usimamizi wa vyombo vya moto kibiashara zinazoongeza uhitaji wa kuwa na Kanuni hizo muhimu zinazolenga kuwasimamia watoa huduma za usafiri na madereva katika usimamizi wa madhara yanayotokana na uchovu wakati wakiendesha vyombo ambavyo vinadhibitiwa na Mamlaka.

"Changamoto ambazo zimeonekana ni kutokuwepo kwa Kanuni mahsusi za kushughulikia na kufanya udhibiti katika usimamizi wa uchovu wa madereva wa vyombo vya usafiri kwa njia ya barabara, kuwepo kwa ongezeko la ajali mbalimbali zinazosababishwa na uchovu wa madereva hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imerushusu mabasi ya abiria kufanya kazi saa 24 na kukosekana kwa nyenzo ya kulinda afya za madereva wa usafiri ardhini ili kuhakikisha wanapata muda wa kutosha kupumzika," amesema Bw. Magombana.

Vilevile amesema, wamiliki wa vyombo vya moto kibiashara wanatakiwa kuandaa mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu kwa lengo la kuimarisha sekta ya usafirishaji.

"Rasimu ya Kanuni hizi zimetoa wajibu kwa madereva na kwa wamiliki wa vyombo katika usimamizi wa madhara ya uchovu ambapo wamiliki wanatakiwa kuandaa mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu na Matarajio ya Serikali ni kwamba, endapo kila mmoja atatimiza kikamilifu

*Inaendelea Uk 16 >>*




*Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa njia ya Barabara Wizara ya Uchukuzi akizungumza na wadau wa usafirishaji katika mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026, ukumbi wa Mikutano Chuo cha Utalii Dar es Salaam Januari 8, 2026.*

# MAGOMBANA: KANUNI HIZI NI MUHIMU KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRISHAJI

*<< Inatoka Uk 15*

wajibu wake kama ilivyoainishwa katika Rasimu ya Kanuni hizi, ubora na usalama wa usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya barabara utaongezeka," ameeleza Bw. Magombana.

Kwa upande wake CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, uchovu wa madereva ni miongoni mwa sababu kubwa zinazosababisha ajali za barabarani ambazo zinagharimu maisha ya watu na mali zao.

"Dereva anapochoka na kuendelea kuendesha gari, hatari ya ajali huwa kubwa na ikitokea tunapoteza uhai wa watu, wengine wanapata ulemavu na taifa linaingia gharama kubwa za matibabu na kupoteza nguvu kazi. Kanuni hizi zinalenga kuweka mifumo madhubuti ya kudhibiti muda wa kazi na mapumziko ya madereva, usimamizi wa ratiba za safari, pamoja na wajibu wa waajiri na wamiliki wa vyombo vya usafiri katika kuhakikisha usalama unazingatiwa," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Vilevile CPA, Dkt. Suluo amesema, Serikali imeona umuhimu wa kuchukua hatua mapema ili kuzuia madhara makubwa yanayotokana na uchovu wa madreva, hususan katika usafiri wa masafa marefu na usafirishaji wa mizigo na kulinda mitaji ya wawekezaji, kulinda afya na usalama wa madereva wao na hasa kulinda uhai wa wananchi .

Rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026, zimeandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na LATRA na zinapatikana kwenye tovuti ya LATRA www.latra.go.tz ambapo wadau wanaweza kuwasilisha maoni yao kwa maandishi kupitia baruapepe group.maoni@latra.go.tz hadi tarehe 22 Januari 2026 ikiwa ni siku 14 baada ya mkutano huo.

# LATRA YAWAKARIBISHA WASAFIRISHAJI KUTOA HUDUMA KUPITIA NJIA YA MOROGORO




CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema Mamlaka imetoa nafasi 150 kwa mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria 26 na kuendelea kutokana na changamoto za usafiri wa mabasi yaendayo haraka maarufu kama mwendokasi kwa njia ya BRT 1 yanayoenda Kimara ili kuongeza huduma za usafiri kwa wananchi kupitia njia hiyo.

CPA Suluo amebainisha hayo Novemba 5, 2025 Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari ambapo amesema wasafirishaji wanapaswa kutuma maombi ya kupata kibali kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) kutoa huduma za usafirishaji kupitia njia ya Morogoro kuanzia Mbezi Luis kwenda Posta, Mnazi Mmoja, Muhimbili na Makumbusho.

Ameongeza kuwa, vibali vitakavyotolewa ni vya muda mfupi wakati marekebisho ya miundombinu yanasubiriwa kukamilika ili kurejesha huduma za usafiri kama ilivyokuwa mwazo.

“Mamlaka inatoa vibali kwa muda wa miezi mitatu kwa sababu tunatarajia kwa kipindi hiki Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) watakuwa wamekamilisha marekebisho ya miundombinu iliyoharibika na kwa njia ya mbagala BRT 2 ambayo ilitolewa kwa muwekezaji MOFAT njia hii haina uharibifu mkubwa wa miundombinu katika mifumo ya ukataji tiketi, marekebisho haya yatakamilika ndani ya muda mfupi na wenzetu DART wakiwa tayari MOFAT atarejea kuendelea kutoa huduma,” ameeleza CPA Suluo.

Akizungumzia huduma za usafiri huo kwa njia ya Mbagala, CPA Suluo amesema kuwa, Mamlaka haitotoa tangazo la kuwakaribisha wasafirishaji wa mabasi ya mijini kutoa



*Inaendelea Uk 18* >>

## LATRA YAWAKARIBISHA WASAFIRISHAJI KUTOA HUDUMA KUPITIA NJIA YA MOROGORO

*<< Inatoka Uk 17*

huduma njia ya Mbagala kwa kuwa tayari idadi ya magari yaliyopo yanajitosheleza na MOFAT akirejea huduma zitaendelea kwa kuwa hali tayari ilishakuwa nzuri.

Novemba 4, 2025 Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliiagiza LATRA kutoa vibali vya muda mfupi kwa mabasi ya mijini ili ziweze kutoa huduma kwa njia ambazo zilikuwa zikitegemea usafiri wa mabasi yaendayo haraka kati ya Gerezani – Kimara na Gerezani – Mbagala.

> **“Mamlaka inatoa vibali kwa muda wa miezi mitatu kwa sababu tunatarajia kwa kipindi hiki Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) watakuwa wamekamilisha marekebisho ya miundombinu iliyoharibika na kwa njia ya mbagala BRT 2 ambayo ilitolewa kwa muwekezaji MOFAT”**
>
> *CPA, Dkt. Habibu Suluo*

---

## MADEREVA WAASWA KUTOTUMIA VILEVI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewaasa madereva wa vyombo vya moto kibiashara kutotumia vilevi ili kuepusha ajali zinazogharimu maisha ya abiria na mali zao.

Amebainisha hayo Bw. Patel Ngereza, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Desemba 11, 2025 kwenye kipindi cha malumbano ya hoja kilichofanyika katika kituo cha habari cha ITV.

“Kanuni za uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu wa vyombo vinavyodibitiwa na LATRA za mwaka 2020 zinamtaka dereva asitumie kilevi chochote pindi anapoendesha basi ama chombo cha moto kibiashara na kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka inafanya kaguzi mbalimbali za kushtukiza kukagua kiwango cha kilevi kwa madereva kabla hawajaanza safari. Wapo baadhi ya madereva wasiojitambua wanatumia vilevi na Mamlaka inaendelea kutoa elimu kwa madereva hao namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwakuwa uhai wa abiria upo mikononi mwao,” amesema Bw. Ngereza.

Vilevile amesema, Mamlaka inatumia mifumo mbalimbali ya kiudhibiti ikiwemo Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) https://vts.latra.go.tz/ unaofuatilia mwenendo wa dereva anapokuwa safarini, Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) https://pis.latra.go.tz/ unaomwezesha abiria kufahamu mwendo na mahali basi lilipo na Mfumo tumizi wa LATRA App unaowezesha kufahamu viwango vya nauli, uhai wa leseni pamoja na makosa ya chombo husika.

Bw. Majura Kafumu, Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva wa Mabasi Tanzania (UWAMATA) amesema chama hicho kinaendelea kuwapatia elimu madereva ili kuhakikisha suala la usalama linazingatiwa huku wakitekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Naye Bw. Juma Libenanga, Mkurugenzi kanda ya Mashariki na Pwani Shirika la Kutetea Haki za Abiria (SHIKUHA) amesema, “Tunashirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa elimu kwa abiria na kuwahimiza kutoa taarifa za uvunjifu wa Sheria, Taratibu na Kanuni za usafiri ardhini wawapo safarini ukizingatia

*Inaendelea Uk 19 >>*

# MADEREVA WAASWA KUTOTUMIA VILEVI

*<< Inatoka Uk 18*

ulevi wa madereva unachangia ajali ambazo zinaepukika," amesema Bw. Libenanga.

Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhiti Usafiri Ardhini (LATRA) Sura ya 413 kimeipa LATRA jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto kibiashara ili kuhakikisha wanakuwa na sifa, uweledi na wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za usafirishaji kwa lengo la kuwezesha ubora wa huduma za usafiri ardhini nchini.

**Kanuni za uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu wa vyombo vinavyodibitiwa na LATRA za mwaka 2020 zinamtaka dereva asitumie kilevi chochote pindi anapoendesha basi ama chombo cha moto**

*Bw. Pateli Ngereza*

---

# MHE. KIHENZILE AIPA HEKO LATRA MATUMIZI YA TEHAMA

Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kazi nzuri inayotekeleza ikiwemo kubuni na kutumia mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imerahisisha upatikanaji wa huduma za usafiri kwa abiria na watumiaji wengine ikiwemo mfumo wa Safari Tiketi unaowezesha ukataji wa tiketi za mabasi yote na tiketi za treni, Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App) unaowezesha taarifa kwa abiria wa mabasi ya mikoani na nchi jirani na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

Mhe. Kihenzile ametoa pongezi hizo Desemba 15, 2025 alipotembelea banda la LATRA katika maonesho ya Mkutano wa 18 wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi unaofanyika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) na kushuhudia shughuli za Udhibiti zinazotekelezwa na LATRA.

Kwa upande wake, CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema kuwa, LATRA imejipambanua kwenye matumizi ya mifumo mbalimbali ya TEHAMA na itaendelea kusimamia utekelezaji wa maono ya viongozi wa Nchi kwa kuongeza ufanisi katika usafirishaji wa abiria na mizigo katika sekta zinazodhibitiwa nchini.

Mkutano huo wa siku tatu unafanyika AICC kuanzia Desemba 15 hadi 17, 2025 ambapo kaulimbiu ni Mifumo Jumuishi ya Usafiri kama Nguzo ya Mageuzi ya Kiuchumi.

# CPA, DKT. SULUO: NAULI ZA DART NI ZA MPITO




CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema Shilingi 1000 wanazotozwa abiria wanaotumia usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) ni nauli ya mpito na nauli halisi zitatumika baada ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuwasilisha maombi ya nauli mpya.

CPA Suluo amebainisha hayo Desemba 17, kwenye Maonesho ya Mkutano wa 18 wa Tathmini ya Utendaji kazi wa Sekta ya Uchukuzi uliofanyika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kuanzia Desemba 15 hadi 17, 2025.

"Nauli ya mpito ya BRT iliridhiwa kuwa shilingi 1,000 kwa Tangazo la Serikali la Agosti 29, 2025 na hii ilikuwa inawapa uhakika wale wanaoleta mabasi kuwa nauli hii wanaweza wakaanza nayo hadi pale DART itakapoleta maombi rasmi ya mapendekezo ya nauli baada ya kukaa na watoa huduma wa usafiri huo. Kwa sasa nauli hizi zinamtosheleza mtoa huduma kutopata hasara lakini kutopata faida ili aingie sokoni na anaweza akaona faida kwa sababu abiria ni wengi, lengo la kuweka nauli hii ni kuwavutia wawekezaji wengine kutoa huduma," amesema CPA Dkt. Suluo.

Pia CPA Suluo ameipongeza DART kwa kutatua changamoto ambazo zilibainika hapo awali na kufanikisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, "Mamlaka ilifanya ziara ya mradi wa BRT awamu ya pili na kabla ya kutangazwa kwa nauli ya shilingi 1,000 kulikuwa na changamoto kwenye uendeshaji ambapo changamoto hiyo ilitatuliwa na huduma za usafiri zikaanza kutolewa. Tunawapongeza na kuwashukuru kwa uboreshaji wa BRT awamu ya pili kwenye mfumo wa kukusanya nauli pamoja na mabasi kuwa mengi hali iliyopelekea mabasi 60 kuazimwa kwenda BTR awamu ya kwanza," amesema CPA. Suluo.

*Inaendelea Uk 21 >>*

## CPA, DKT. SULUO: NAULI ZA DART NI ZA MPITO

*<< Inatoka Uk 20*

Kwa upande wake Bw. Said Tunda, Mtendaji Mkuu DART amesema kuwa, "Serikali inawajali sana wananchi wake ndio maana hata baada ya kuharibika miundombinu iliyosababisha changamoto ya usafiri kwa wananchi, huduma zinaendelea katika vituo vingi vya mwendokasi kwa kulipia gharama ya shilingi 1,000 tu ambapo ni ongezeko la shilingi 250 kutoka nauli ya awali," amesema Bw. Tunda.

Aliongeza kuwa, nauli ya shilingi 1,000 inafaa kwa kuanzia kwani lengo sio kuwaumiza watumia huduma bali ni kuhakikisha abiria wanapata huduma bora na endelevu kwani wakati huduma za BRT hazipo, abiria walikuwa wanatozwa hadi shilingi 6,000 kwa safari moja walipotumia vyombo vidogo vya usafiri.

Kwa mujibu wa Kanuni za LATRA za Tozo za mwaka 2020, watoa huduma wanatakiwa kutoa matangazo ya nauli mpya kwa siku kumi na nne (14) kabla ya kuanza kutumia nauli mpya kupitia vyombo vya habari vinavyowafikia watu wengi.

---

## VIBALI VYA DHARURA 169 VYATOLEWA, MSONGAMANO WAPUNGUA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa jumla ya vibali 169 vya safari kwa mabasi yanayosafiri kuanzia Dar es Salaam kuelekea mikoa mbalimbali Tanzania Bara kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za usafiri kwa abiria kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka 2025.

Hayo yamebainishwa Desemba 15, 2025 na Bi. Rukia Kibwana, Afisa Mfawidhi LATRA Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli Dar es Salaam ambapo amesema vibali hivyo vya muda hutolewa mwisho wa mwaka kutokana na ongezeko la abiria wanaosafiri kwenda mikoani.

"Kuanzia Novemba 30, 2025 hadi kufikia leo jumla ya vibali 169 vimetolewa katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa mabasi yanayosafiri mikoa mbalimbali nchini, vibali hivyo vimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongano wa abiria kituoni hapa kwa nyakati tofauti hasa nyakati za asubuhi na jioni ambapo abiria ni wengi zaidi," amesema Bi. Kibwana.

Bi. Kibwana ameeleza kuwa awali Mamlaka ilianza kwa kutoa vibali 72 kwa mikoa ya Iringa, Dodoma, Morogoro na Tanga ambapo uhitaji wa safari za abiria ulionekana kuwa ni mkubwa.

Pia ameeleza vigezo vilivyozingatiwa kutoa vibali hivyo ni, mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria 40 na kuendelea au iwe na leseni ya Mabasi Maalum ya Kukodi (Special Hire), basi liwe limeunganishwa kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), dereva awe na Kitufe cha Utambuzi (i-Button) kilichosajiliwa na LATRA na basi liwe limeunganishwa kwenye Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaojulikana kwa jina la Safari Tiketi.

Aidha Bi. Kibwana amesema, Mamlaka imewataka wananchi kuendelea kuwa na uvumilivu katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka akifafanua kuwa, LATRA inafahamu idadi kubwa ya uhitaji kwa abiria hivyo

*Inaendelea Uk 22 >>*

## VIBALI VYA DHARURA 169 VYATOLEWA, MSONGAMANO WAPUNGUA

*<< Inatoka Uk 21*

inaendelea kusimamia na kuratibu huduma za usafiri kwa kuongeza vibali vya usafiri.

Mamlaka imekuwa na utaratibu unaofanyika kila mwaka kutoa vibali vya muda inapofika kipindi cha mwisho wa mwaka kuelekea sherehe za Krismas na Mwaka mpya kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za usafiri kwa abiria unaimarika.

> **“Kuanzia Novemba 30, 2025 hadi kufikia leo jumla ya vibali 169 vimetolewa katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa mabasi yanayosafiri mikoa mbalimbali nchini**
>
> ***Bi. Rukia Kibwana***

---

## CPA, SULUO AWASIHI WADAU KUITUNZA AMANI




CPA, Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi wadau wa sekta ya usafiri ardhini wakiwemo wasafirishaji, watoa huduma na watanzania wote kuungana pamoja kuilinda, kuitunza na kuienzi amani ya nchi na pia amewasihi wanahabari kutoa habari zinazowaleta watanzania pamoja na zinazolenga kudumisha amani.

CPA Suluo amebainisha hayo Oktoba 08, 2025 ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja yanayofanyika Oktoba 06 hadi 10, 2025 yenye kaulimbiu “Mission: Possible” yaani Mipango Imewezakana.

“Tunawashukuru wadau wetu kwa kuwa nasi bega kwa bega katika kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji nchini na tunafurahi tunasherehekea pamoja wiki hii ya huduma kwa wateja tukiwa na amani na utulivu. Niwakumbushe kuwa nchi yetu inaelekea kwenye kipindi cha uchaguzi mkuu, nawasihi tuenzi amani ya nchi yetu, tudumishe umoja na mshikamano wetu kama watanzania na tarehe 29 tujitokeze kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura tulivyojiandikisha ili tukatumie haki yetu ya kikatiba kwa kupiga kura kwa amani,” amesisitiza CPA Suluo.

Katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, CPA Suluo alishiriki kikamilifu kutoa huduma, kusikiliza maoni na kutatua changamoto za wateja waliotembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

*Maafisa wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakitoa elimu kwa wadau mbalimbali wa usafiri ardhini kuhusu majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka kwenye Maonesho ya Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025 viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam Novemba 25, 2025.* >>





<< 1. *Muwezeshaji kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma akitoa mafunzo kwa Waelimisha rika kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuhusu utekelezaji wa afua za Virusi vya Ukimwi (VVU) na magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahali pa kazi. Mafunzo hayo yametolewa Jijini Dodoma Octoba 23, 2025.*

*CPA, DKT. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA kwenye kikao cha watoa huduma za Usafiri Ardhini na waandishi wa habari akizungumzia kuhusu tuzo za watoa huduma bora na salama mwaka 2025 zitakazotolewa kwenye Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025. Ofisi za LATRA Dar es Salaam Novemba 12, 2025.* >>



# CPA, DKT. SULUO: TUZO TULIYOIPATA NI CHACHU YA KUWAHUDUMIA ZAIDI WATANZANIA




*Mhe. Joseph Mkude (Wa katikati), Mkuu wa Wilaya ya Arusha, kwa niaba ya Mhe. Prof. Makame Mbarawa Waziri wa Uchukuzi akimkabidhi Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA tuzo ya LATRA, Mshindi wa Kwanza kwa utendaji kazi mwaka 2024/25 katika Mkutano wa Mwaka wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi, Desemba 17, 2025 jijini Arusha*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeibuka mshindi wa kwanza miongoni mwa Taasisi za Wizara ya Uchukuzi zilizofanya vizuri kiutendaji kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambapo CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema tuzo hiyo ni chachu ya kuwahudumia zaidi watanzania kwa kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini.

Tuzo hiyo imetolewa na Mhe. Joseph Mkude, Mkuu wa Wilaya ya Arusha aliyemuwakilisha Mgeni Rasmi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi na kupokelewa na Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA katika kilele cha Mkutano wa 18 wa Mwaka wa Tathmini ya Utendaji kazi wa Sekta ya Uchukuzi, Desemba 17, 2025 Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

CPA, Dkt. Suluo amesema kuwa, hivi karibuni Mamlaka imepata ithibati ya kimataifa ya ubora wa huduma (ISO 9001) na hivyo itaendelea kuboresha huduma zake ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za usafiri ardhini, kuwawezesha wasafirishaji na watoa huduma kutekeleza majukumu yao kwa uhuru bila kuwakwaza.

Vilevile amesema kuwa, Mamlaka inapaswa kuutunza ushindi huo, "Tumekuwa washindi wa kwanza kwa mara nyingine tumeendelea kutunza nafasi yetu ya ushindi na hii ni kwa namna ambavyo tumejipanga, tunajituma, tunashirikiana na pia tunashirikisha wadau katika uamuzi tunaofanya tunapotekeleza majukumu yetu ili kuacha nyuso za tabasamu kwa watanzania haswa katika sekta hii ya usafiri ardhini," ameeleza CPA ,Dkt. Suluo.

Ameongeza kuwa, tuzo hiyo ni ishara kuwa LATRA inatekeleza maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutafsiri maono yake kwa vitendo kwa kutekeleza kazi na

*Inaendelea Uk 25 >>*

# CPA, DKT. SULUO: TUZO TULIYOIPATA NI CHACHU YA KUWAHUDUMIA ZAIDI WATANZANIA

*<< Inatoka Uk 24*

majukumu kwa ufanisi kwa watanzania ambao ni watumiaji wa huduma za usafiri ardhini nchini.

Vilevile ameishukuru Wizara ya Uchukuzi inayoongozwa na Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi na uongozi mzima wa Wizara, pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA inayoongozwa na Prof. Ahmed Mohamed Ame. Mwenyekiti wa Bodi hiyo kwa kuisimamia Menejimenti na wafanyakazi wote wa Mamlaka na kuhakikisha Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa uweledi na ufanisi.

Tuzo hiyo ya utendaji kazi bora kwa taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Uchukuzi ni muendelezo wa ushindi kwa Mamlaka ambapo LATRA imekuwa ikishika nafasi ya kwanza kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2022/23, 2023/24, na kwa mwaka huu wa fedha 2024/25.



IMETHIBITISHWA ISO 9001

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), likiongozwa na Bodi ya Wahariri;**

Mwenyekiti: **CPA DKT. HABIBU SULUO** | Mhariri Mkuu: **SAMUEL KEENJA** | Wahariri Wasaidizi: **SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE** | Waandishi: **MAMBWANA JUMBE, MARYAM NINA** na **NANCY AMANI** | Wasanifu Jarida: **DEUSDEDITY MASEMBA** na **IBRAHIM SAID**

**©2025**